BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2018

# 06 URAIA NA MAADILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2018

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA SWALI 2

2.1 Sehemu A (Alama 26) .......... 2
2.2 Sehemu B (Alama 24) .......... 16

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI .......... 31

4.0 HITIMISHO .......... 32

5.0 MAPENDEKEZO .......... 32

Kiambatisho A .......... 34

Kiambatisho B .......... 35

## DIBAJI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera na wadau wengine wa elimu kuhusu maarifa, stadi na mielekeo ambayo wanafunzi waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi. Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2018 katika somo hili umetayarishwa kwa mara ya kwanza kwa kuzingatia mabadiliko ya Mtaala wa Elimu ya Msingi kwa Darasa la III hadi IV wa mwaka 2016. Hivyo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu unaweza kutumika kama kipimo cha ufanisi katika utekelezaji wa mtaala huo kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu inayowajengea wanafunzi uwezo katika umahiri mbalimbali wa somo la Uraia na Maadili.

Katika taarifa hii, umahiri wa wanafunzi waliopata katika dhana mbalimbali umeainishwa. Aidha changamoto mbalimbali ambazo zimechangia wanafunzi kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi zimeainishwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa umahiri mbalimbali, na kushindwa kuhawilisha maarifa. Aidha, mwishoni mwa taarifa hii kuna kiambatisho kinachoonesha jinsi wanafunzi walivyofaulu katika kila umahiri uliopimwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zitapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa ya wanafunzi.

Mwisho, Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde

KATIBU MTENDAJI

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe 23 mwezi Novemba mwaka 2018. Upimaji huu umetokana na muhtasari mpya ambao umelenga katika kuwajengea wanafunzi umahiri ambao utapimwa kupitia Utendaji wa wanafunzi katika kubaini maarifa, stadi na mwelekeo walionao katika kufikia umahiri mahsusi ulioainishwa. Hivyo viwango vya utendaji wa wanafunzi katika upimaji huo vimegawanyika katika makundi manne; **Kiwango hafifu**, **Kiwango cha wastani**, **Kiwango kizuri** na **Kiwango kizuri sana**. Wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu walihesabika kufeli na wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani hadi utendaji mzuri sana walihesabika kufaulu upimaji huo.

Jumla ya wanafunzi **1,362,523** walijiandikisha kufanya upimaji ambapo wanafunzi **1,301,324** walifanya upimaji huu. Aidha, kufaulu kwa wanafunzi katika somo hili kunaonesha kuwa wanafunzi **1,207,664** sawa na asilimia **92.80** walifaulu, na wanafunzi **93,660** sawa na asilimia **7.2** hawakufaulu.

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulikuwa na jumla ya maswali 6 yenye jumla ya vipengele 25. Upimaji huu uligawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 13 ambavyo vilikuwa na jumla ya alama 26 na sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 12 ambavyo vilikuwa na jumla ya alama 24. Kwa ujumla upimaji ulikuwa na alama 50 na wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote A na B.

Katika sehemu A, wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku, kuoanisha majukumu yaliyoainishwa katika fungu A na vyeo vya wahusika wa majukumu hayo katika fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi, na kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Aidha, katika sehemu B, wanafunzi walitakiwa kuweka alama ya vema kwenye sehemu inayohusika, kuchunguza picha kisha kujibu maswali, na kusoma kwa umakini kifungu cha habari na kujaza sehemu zilizoachwa wazi.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa somo la Uraia na Maadili imejikita katika kuangalia maswali yote sita yaliyotoka katika umahiri mbalimbali ulioainishwa katika muhtasari. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuchagua jibu sahihi na sababu zilizofanya wachague majibu hayo.

Viwango vya kufaulu kwa kila swali vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu swali husika. Iwapo asilimia 0 **-** 33 waliweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango cha kufaulu kwa swali hilo kilihesabika kuwa ni **hafifu***.* Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 - 66 kufaulu kwa swali hilo kulihesabika kuwa ni kwa **wastani** na kiwango cha kufaulu kilihesabika kuwa ni **kizuri** iwapo wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 – 100. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatishwa ili kufafanua kufaulu kwa wanafunzi ambapo rangi ya kijani inawakilisha kufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kufaulu kwa kiwango cha wastani na kufaulu kwa kiwango hafifu kunawakilishwa na rangi nyekundu.


## 2.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A (Alama 26)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo Swali la 1 lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi lenye jumla ya alama 10, Swali la 2 la kuoanisha lenye jumla ya alama 8 na Swali la 3 la kuchagua jibu sahihi na kuandika katika mabano lenye jumla ya alama 8. Jumla ya alama katika sehemu hii ni 26. Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika sehemu hii.

**Swali 1:** Swali hili lilikuwa na vipengele vitano vya kuchagua jibu sahihi vilivyotoka katika Umahiri wa *Kuthamini Jamii*. Kila kipengele kwenye swali hili kilikuwa na jumla ya alama 02. Jumla ya wanafunzi 1,301,580 walifanya swali hili ambapo wanafunzi 538392 (41.4%) walifanya vizuri sana kwa kupata alama zote 10, wanafunzi 359598 (27.6%) walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama 8, wanafunzi 314341

(24.1%) walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa kupata alama 4 hadi 6, na wanafunzi 89249 (6.9%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama 0 au 2. Kwa ujumla ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni mzuri kama inavyoonekana katika **Chati Na. 1**.




**Chati Na. 1:** *inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 93.2 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata alama 4 hadi 10.*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye skripti za wanafunzi unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi walichagua majibu sahihi na wengine walivutiwa na vipotoshi kutokana na sababu mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye uchambuzi wa kila kipengele.

(i) Lipi kati ya matendo yafuatayo linachangia katika uchafuzi wa vyanzo vya maji?

A. Ufugaji wa kisasa

B. Kuchota maji mtoni

C. Kuoga mtoni

D. Kuvuna maji ya mvua.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kutunza Mazingira na Vilivyomo*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini tabia na mienendo inayosababisha uharibifu wa mazingira katika jamii. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi C, *Kuoga mtoni* walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya matendo yanayochangia katika uchafuzi wa vyanzo vya maji, hivyo ilikuwa rahisi kwao kuhawilisha maarifa. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa maji ni muhimu kwa maisha ya watu, mimea na wanyama na ni rasilimali muhimu inayopaswa kutumiwa kwa uangalifu na kutunzwa. Vilevile walibaini kuwa kuoga mtoni ni moja ya matendo yanayochafua maji.

Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi A, *Ufugaji wa kisasa*; B, *Kuchota maji mtoni*, na D, *Kuvuna maji ya mvua* hawakuwa na elimu ya utunzaji wa mazingira. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Ufugaji wa kisasa*, walichanganya kati ya ufugaji wa kisasa na kienyeji. Hawakufahamu kuwa ufugaji wa kisasa ni ufugaji unaozingatia kanuni za utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, ambapo mifugo huwekwa kwenye sehemu maalumu kama vile banda au ndani ya uzio pasipo kuathiri mazingira na vyanzo vya maji.

Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi B, *Kuchota maji mtoni* na D, *Kuvuna maji ya mvua* walishindwa kuelewa kuwa kuchota maji mtoni na kuvuna maji ya mvua sio vitendo vyenye kuharibu maji bali ni vitendo salama katika utunzaji wa maji na vyanzo vyake. Mtu anapochota maji mtoni anatumia ndoo au chombo kama bakuli na kuvuna maji ya mvua hufanyika kwa vifaa maalumu kama vile ndoo, pipa au bwawa.

(ii) Ipi kati ya tabia zifuatazo inaleta uharibifu wa mazingira?

A. Matumizi ya mbolea ya samadi
B. Kukata miti ovyo
C. Kumwagilia bustani maji
D. Kufyeka nyasi.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kutunza Mazingira na Vilivyomo*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini

tabia mbalimbali za uharibifu wa mazingira katika jamii. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *Kukata miti ovyo* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tabia zinazosababisha uharibifu wa mazingira katika jamii. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa uharibifu wa mazingira husababishwa na tabia, mienendo na vitendo visivyofaa vya binadamu kama kukata miti ovyo, kufuga mifugo mingi kama ng'ombe na mbuzi bila kuwa na eneo la malisho na uchomaji holela wa miti au misitu kwa ajili ya mkaa, kuwinda na shughuli za kilimo.

Wanafunzi wachache walivutiwa na vipotoshi A, *Matumizi ya mbolea ya samadi*; C, *Kumwagilia bustani maji* na D, *Kufyeka nyasi*. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Matumizi ya mbolea ya samadi*, walishindwa kuelewa kuwa mbolea ya samadi ni muhimu sana katika kustawisha mimea mbalimbali katika mazingira yetu. Wanafunzi hao walidhani kinyesi cha wanyama kinachafua mazingira na si kustawisha mimea. Wanafunzi waliochagua vipotoshi C, *Kumwagilia bustani maji* na D, *Kufyeka nyasi* hawakuwa na uelewa kuhusu vitendo au stadi za utunzaji wa mazingira. Hawakuelewa kuwa kumwagilia bustani maji ni kitendo cha kuthamini mazingira na mimea ili istawi, na kufyeka nyasi ni kitendo cha kutunza na kusafisha mazingira ili yawe bora na kuepuka madhara yatokanayo na mazingira machafu kama kung'atwa na wadudu wanaotambaa.

(iii) Ni faida gani inatokana na matumizi ya chandarua wakati wa kulala?

A. Kuzuia ugonjwa wa kifua kikuu
B. Kuzuia ugonjwa wa malaria
C. Kuzuia ugonjwa wa kipindupindu
D. Kuzuia baridi wakati wa usiku.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali Wengine*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini vitendo/tabia hatarishi kwa afya yake, familia na jamii kama kulala bila ya kutumia chandarua.

Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi B, *Kuzuia ugonjwa wa malaria,* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matendo ya mtu kujijali kama kutumia chandarua wakati wa kulala. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuhusu faida zitokanazo na matumizi sahihi ya chandarua wakati wa kulala na athari za kutotumia chandarua wakati wa kulala ikiwa ni pamoja na kung'atwa na mbu waenezao ugonjwa wa malaria.

Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi A, *Kuzuia ugonjwa wa kifua kikuu* na C, *Kuzuia ugonjwa wa kipindupindu* ni dhahiri kuwa hawakuwa na uelewa juu ya magonjwa mbalimbali na jinsi yanavyoambukizwa. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kuzuia baridi wakati wa usiku* hawakuwa na maarifa kuwa chandarua ni neti inayoning'inizwa na kuzungushwa juu ya kitanda kwa ajili ya kuwazuia mbu wasimfikie mtu aliyelala. Pia wanafunzi hao hawakuwa na uelewa kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua.

(iv) Kitendo cha baadhi ya watoto kuzurura mitaani ni kiashiria cha

A. tabia ya unafiki.
B. tabia ya majungu.
C. tabia ya tamaa.
D. tabia hatarishi.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali wengine*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wake na familia yake. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi D, *tabia hatarishi* walionesha umahiri katika kubaini matendo yanayoweza kuwasababishia madhara kama kuzurura mitaani, kupokea vitu kutoka kwa watu wasiowafahamu, kutozingatia kanuni za usafi wanapotoka chooni na kitendo cha kuwa na marafiki wabaya kama wezi.

Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua vipotoshi A, *tabia ya unafiki*; B, *tabia ya majungu* na C, *tabia ya tamaa* walishindwa kuelewa maana halisi ya vitendo hivi kuwa tabia ya unafiki ni dai la uongo au la kujifanya kuwa unafuata taratibu, misingi ya uadilifu, urafiki

au imani ilihali ni kinyume chake. Majungu ni ile tabia ya mtu kusambaza maneno yasiyo ya kweli au tabia ya kutoa taarifa ya uongo, na tabia ya tamaa ni hamu kubwa ya kufanya jambo na matarajio ya kupata kitu hata ikiwa si kwa njia halali.

(v) Ni kwa nini watoto wanashauriwa kukataa kupokea fedha au zawadi kutoka kwa watu wasiowajua?

A. Kuzuia utajiri

A. Kuzuia uzururaji

B. Kuepuka vishawishi

C. Kuepuka uvivu.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali Wengine* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuepuka vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wao na jamii kwa ujumla. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi C, *Kuepuka vishawishi* walionesha kuwa na maarifa kuhusu vitendo vya kutojijali ambavyo hupelekea vishawishi. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa kupokea fedha au zawadi kutoka kwa watu wasiowajua ni tabia ya kushawishika ambayo inaweza kuwa na madhara katika maisha yao ya kila siku hasa kwa wanafunzi wa kike ambao hushawishiwa kwa zawadi au fedha ili kuingizwa katika tabia za kupenda ngono.


Wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi kwa kuchagua kipotoshi A, *Kuzuia utajiri* walikosa maarifa kuwa utajiri haupatikani kwa njia ya kupewa fedha au zawadi na watu wasiowajua; bali utajiri unakuja kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwa na maamuzi sahihi. Aidha, wanafunzi waliovutiwa na vipotoshi B, *Kuzuia uzururaji* na D, *Kuepuka uvivu* walishindwa kutambua kuwa vitendo vya kuzuia uzururaji na kuepuka uvivu havina uhusiano na athari za kupokea zawadi au fedha kutoka kwa watu wasiowajua.

**Swali la 2:** Swali hili liliwataka wanafunzi kujibu kipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha majukumu yaliyoainishwa katika **Fungu A** na vyeo vya

wahusika wa majukumu hayo katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Husimamia mahudhurio na taaluma darasani pamoja na nidhamu. | ( ) | A. Kamati ya shule<br>B. Mwalimu wa darasa<br>C. Mwalimu wa taaluma<br>D. Mwalimu mkuu<br>E. Mwalimu wa nidhamu<br>F. Kiranja mkuu |
| (ii) Hupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule. | ( ) | |
| (iii) Husimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kuhakikisha kuwa wamevaa sare za shule. | ( ) | |
| (iv) Husimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule za kila siku. | ( ) | |

Swali lilitoka katika umahiri mkuu *Kuheshimu Jamii* kwenye umahiri mahususi wa *Kuipenda shule yetu*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini muundo wa uongozi wa shule na majukumu ya kila kiongozi. Kila kipengele katika swali kilikuwa na jumla ya alama 2. Kwa ujumla kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwa kuwa asilimia 54.9 ya wanafunzi wote 1,301,577 waliofanya swali hili walipata alama 0 au 2. Kiwango hiki cha kufaulu ni cha chini ikilinganishwa na maswali mengine katika somo hili ambapo asilimia 45.1 pekee ya wanafunzi waliofanya swali hili walifaulu kwa kupata kiwango cha wastani hadi kizuri sana. **Chati Na. 2** inaonesha takwimu za ufaulu katika Swali la 2.




**Chati Na. 2:** *inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 45.1 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata alama 4 hadi 8.*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa sababu mbalimbali ziliwafanya wanafunzi kubaini/kushindwa kubaini majibu sahihi kama inavyooneshwa katika uchambuzi ufuatao:

Kipengele (i) kilipima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini majukumu ya kiongozi wa shule anayesimamia mahudhurio na taaluma darasani pamoja na nidhamu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *Mwalimu wa darasa* walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muundo wa uongozi wa shule na majukumu ya kila kiongozi. Wanafunzi hao waliweza kubaini kuwa mwalimu wa darasa ndiye anayesimamia mahudhurio, taaluma na nidhamu darasani. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kamati ya shule* hawakuelewa kuwa kamati ya shule hupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule na si kusimamia mahudhurio, taaluma na nidhamu ya wanafunzi darasani. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi C, *Mwalimu wa taaluma* walishindwa kutambua kuwa Mwalimu wa taaluma husimamia shughuli zote za kitaaluma shuleni kama vile kuandaa ratiba, mitihani na majaribio. Aidha, wanafunzi wengi walivutiwa na kipotoshi D, *Mwalimu mkuu* kwa sababu hawakuzifahamu vizuri kazi za Mwalimu mkuu ambazo ni kusimamia shughuli za kila siku za shule. Wanafunzi waliochagua kipotoshi E, *Mwalimu wa nidhamu* walishindwa kutofautisha majukumu ya Mwalimu wa darasa na Mwalimu wa nidhamu, kwa kuwa mwalimu

wa darasa anashughulikia nidhamu ya wanafunzi darasani na mwalimu wa nidhamu anashughulikia nidhamu shuleni. Wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Kiranja mkuu* hawakuelewa kuwa Kiranja mkuu ni kiongozi wa wanafunzi anayesimamia majukumu yote yanayowahusu wanafunzi na ni msimamizi wa viranja wengine.


Kipengele cha (ii) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua cheo cha viongozi wa shule ambao jukumu lao ni kupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule. Wanafunzi waoliweza kujibu swali hili kwa usahihi walichagua na kuandika herufi ya jibu sahihi A, *Kamati ya shule.* Wanafunzi hao walitambua kuwa kamati ya shule ni kiungo muhimu katika shule na jamii inayowazunguka na jukumu lake ni kupanga na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule. Wanafunzi wengine waliovutiwa na vipotoshi B, *Mwalimu wa darasa;* C, *Mwalimu wa taaluma;* D, *Mwalimu mkuu;* E, *Mwalimu wa nidhamu* na F, *Kiranja mkuu* hawakuwa na uelewa kuhusu muundo wa uongozi wa shule jambo lililowafanya washindwe kutofautisha majukumu ya Kamati ya Shule na ya viongozi wengine wa shule.

Kipengele cha (iii) kilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini cheo cha kiongozi wa shule ambaye jukumu lake ni kusimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanavaa sare za shule. Wanafunzi walioweza kujibu swali hili kwa usahihi walichagua na kuandika herufi ya jibu sahihi E, *Mwalimu wa nidhamu*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya majukumu ya mwalimu wa nidhamu kwani waliweza kubaini kuwa mwalimu wa nidhamu ndiye anayesimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kuhakikisha kuwa wamevaa sare za shule. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kamati ya shule* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya Kamati ya shule ambayo ni kusimamia mipango yote ya maendeleo katika shule. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Mwalimu wa darasa* walishindwa kubaini kuwa mwalimu wa darasa husimamia nidhamu ya wanafunzi darasani na si shule nzima kama mwalimu wa nidhamu. Wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi C, *Mwalimu wa taaluma* hawakuelewa kuwa mwalimu wa taaluma husimamia taaluma shuleni. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Mwalimu mkuu* hawakuelewa kuwa Mwalimu mkuu husimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule

za kila siku. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Kiranja mkuu* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya majukumu ya viranja wa shule.

Kipengele (iv) kilipima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini cheo cha kiongozi wa shule ambaye jukumu lake ni kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule za kila siku. Wanafunzi waliojibu swali hili kwa usahihi walichagua na kuandika herufi ya jibu sahihi D, *Mwalimu mkuu*. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya *Mwalimu mkuu* ambayo ni kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa shule za kila siku ikiwa ni pamoja na kuhakikisha walimu wanafundisha ipasavyo, nidhamu nzuri ya wanafunzi na mazingira safi na salama ya wanafunzi kujifunza. Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *kamati ya shule* walishindwa kutofautisha majukumu ya *Mwalimu mkuu* na *Kamati ya shule* kwa sababu *Mwalimu mkuu* ni katibu katika kamati hiyo. Wanafunzi wengine waliochagua vipotoshi B, *Mwalimu wa Darasa* C; *Mwalimu wa taaluma* na E, *Mwalimu wa nidhamu* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muundo wa uongozi wa shule na majukumu ya kila kiongozi. Aidha wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Kiranja mkuu* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya majukumu ya Kiranja mkuu wa shule.

**Swali la 3**: Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kuwa Mwajibikaji*. Swali lilimtaka wanafunzi kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne vilivyotoka katika umahiri mahususi mbalimbali na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kuzuri kwani asilimia 79.1 ya wanafunzi waliweza kupata alama 4 hadi 8, na wanafunzi wachache (20.9%) walishindwa kwa kupata alama 0 au 2 ambacho ni kiwango hafifu. **Chati Na. 3** inaonesha takwimu za kufaulu kwa wanafunzi katika Swali la 3.




**Chati Na. 3**: *inaonesha ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 79.1 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata kiwango cha wastani hadi kizuri sana.*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye skripti za wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kuandika majibu sahihi katika vipengele vyote na wachache walishindwa kwa sababu mbalimbali kama inavyooneshwa katika uchambuzi ufuatao:

(i) Kitendo cha kumwambia mtu alichokifanya sio sahihi ni

________________________________

(kumuadhibu, kumkosoa, kudanganya)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kutii Sheria na Kanuni katika Kutekeleza Majukumu yake Kila Siku*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini maana sahihi ya vitendo vya kukemea na kukosoa/visivyo sahihi vinavyoashiria ukiukwaji wa kanuni. Wanafunzi walioweza kuchagua na kuandika jibu sahihi *kumkosoa* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matendo yanayotakiwa kukemewa na kukosolewa kama ukiukaji wa kanuni za shule, barabarani na za usafi ambazo huweza kupelekea madhara kama vile kupata maradhi, kupata majeraha na pengine kufa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliokosa swali hili walichagua vipotoshi *kumuadhibu* na *kudanganya* kwa kudhani kuwa kitendo cha kumwambia mtu ukweli ni kumuadhibu au kumdanganya. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa kutokumwambia mtu ukweli ikiwa kweli katenda uovu ni tabia mbaya ya unafiki. Tabia ya unafiki ni dai la uongo au la kujifanya kuwa unafuata taratibu, misingi ya uadilifu, urafiki au imani ilihali ni kinyume chake. Walishindwa kuelewa kuwa vitendo vya ukiukwaji wa kanuni au visivyo sahihi vinavyotendeka katika jamii ni vitendo vya kufichuliwa na kukemewa ipasavyo.

(ii) Kufanya kazi kwa pamoja inamaanisha ____________________

(kushirikiana, kubaguana, kuchukiana)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kushirikiana Katika Kutekeleza Majukumu ya Nyumbani na Shuleni*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua maana ya kitendo na tabia ya kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni. Wanafunzi waliochagua na kuandika jibu sahihi *kushirikiana* walionesha ufahamu mkubwa juu ya matendo ya kushirikiana wanayoyafanya katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi *kubaguana* na *kuchukiana* hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya vitendo vya kushirikiana. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa kubaguana na kuchukiana ni athari za kutokushirikiana. Wanafunzi hao hawakufahamu kuwa kubaguana ni kitendo cha kumtenga mtu kwa kufuata misingi fulani na kuchukiana ni kitendo cha kujenga uhasama na mtu, kitu au jambo.

(iii) Kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni ____________________

(ubinafsi, nidhamu binafsi, woga)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kuwa na Nidhamu Binafsi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kudadisi mambo mbalimbali na kujiwekea malengo kwa kila jambo analotaka kutenda. Katika swali hili wanafunzi walioweza kuchagua na kuandika jibu sahihi *nidhamu binafsi* walionesha kuwa na uwezo mkubwa wa kudadisi mambo.

Wanafunzi hao walitambua kuwa kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni kitendo cha kuwa na nidhamu binafsi ambayo ni uwezo wa kutenda jambo bila kusimamiwa na mtu mwingine.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliokosa swali hili walichagua vipotoshi *ubinafsi* na *woga* kwa kudhani kuwa mtu hawezi kufanya mambo yake mwenyewe bila kusimamiwa na mtu mwingine kama mwalimu au mzazi. Wanafunzi hao pia hawakuelewa kuwa ubinafsi ni tabia ya mtu kujithamini na kujijali mwenyewe pasipo kujali maslahi ya wengine wakati woga ni hisia za kujawa na hofu ya kupatwa na jambo baya usilolimudu. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kuandika majibu yasiyo na uhusiano na swali.

(iv) Nini hutumika kudhibiti tabia za wanafunzi shuleni?

________________________________________

(nembo ya shule, mipaka ya shule, sheria za shule)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi *Kutii Sheria na Kanuni katika Kutekeleza Majukumu yake Kila Siku* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini vitendo vinavyoashiria uwepo wa sheria na kanuni katika mazingira ya shule. Wanafunzi waliochagua na kuandika jibu sahihi *sheria za shule* walikuwa na ufahamu kuwa, ili wanafunzi waweze kujifunza vizuri masomo yao na kufikia malengo yaliyopangwa ni lazima kutii sheria na kanuni zinazowaongoza katika shughuli za kila siku za shule.

Wanafunzi waliokosa swali hili walichagua vipotoshi *nembo ya Shule* na *mipaka ya shule* kwa kudhani kuwa nembo ya shule ni kidhibiti kizuri cha wanafunzi kwa kuwa inawakilisha picha, jina na kauli mbiu ya shule. Pia walidhani kudhibiti tabia za mwanafunzi shuleni ni sawa na udhibiti wa mipaka ya shule. Walishindwa kuelewa kuwa mipaka ya shule ni mistari ya kufikirika au alama zinazoonesha mwisho wa eneo la shule tu na halina uhusiano na kudhibiti tabia za mwanafunzi. Wanafunzi hao pia hawakuwa na ufahamu kuhusu umuhimu wa kufuata na kuzingatia sheria na kanuni za shule.

**Kielelezo Na. 3.1** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika majibu sahihi katika swali hili.

**Kielelezo Na. 3.1**

3. Jibu kipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kitendo cha kumwambia mtu alichokifanya sio sahihi ni

Kumkosoa

(kumuadhibu, kumkosoa, kudanganya)

(ii) Kufanyakazi kwa pamoja inamaanisha Kushirikiana.

(kushirikiana, kubaguana, kuchukiana)

(iii) Kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni

Nidhamu binafsi.

(ubinafsi, nidhamu binafsi woga)

(iv) Nini hutumika kudhibiti tabia za wanafunzi shuleni?


Sheria za Shule.

(nembo ya shule, mipaka ya shule, sheria za shule)

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeelewa matakwa ya swali na kuandika majibu sahihi kwa kila kipengele.

Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kuchagua na kuandika majibu sahihi kama ilivyochambuliwa katika kipengele (i) – (iv). **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo Na. 3.2**



3. Jibu kipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kitendo cha kumwambia mtu alichokifanya sio sahihi ni Sahihi
(kumuadhibu, kumkosoa, kudanganya)

(ii) Kufanyakazi kwa pamoja inamaanisha ndio
(kushirikiana, kubaguana, kuchukiana)

(iii) Kufanya mambo mazuri uliyojipangia ni

kujisomea na kuandika
(ubinafsi, nidhamu binafsi, woga)

(iv) Nini hutumika kudhibiti tabia za wanafunzi shuleni?

kujisomea
(nembo ya shule, mipaka ya shule, sheria za shule)

**Kielelezo Na. 3.2:** Kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali. Mwanafunzi alitoa majibu yake badala ya kuchagua kwenye mabano na hivyo kukosa vipengele vyote.

## 2.2 Sehemu B (Alama 24)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) swali la 4, 5, na la 6. Swali la 4 lilikuwa la kuonesha matendo yanayoonesha haki au wajibu kwa kuweka alama ya vema (√ ) kwenye sehemu inayohusika, na lilikuwa na jumla ya alama 8. Swali la 5 lilikuwa la kuchunguza picha kisha


kujibu maswali yanayofuata na lilikuwa na alama 8, na swali la 6 lilikuwa la kusoma kifungu cha habari kisha kujibu kipengele i - iv katika sehemu zilizoachwa wazi na lilikuwa na alama 8. Jumla ya alama katika sehemu hii ni 24. Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika sehemu hii.

**Swali la 4:** Swali hili liliwataka wanafunzi kujibu kipengele (i) - (iv) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **haki** au **wajibu** kwa kuweka **alama ya vema (√)** kwenye **sehemu** inayohusika. Namba **(i)** imetolewa **kama mfano**.

| **Na.** | **Matendo** | **Haki** | **Wajibu** |
|---|---|---|---|
| (i) | Kulindwa. | √ | |
| (ii) | Kucheza michezo mbalimbali. | | |
| (iii) | Kuwasaidia wakubwa na wadogo zako. | | |
| (iv) | Kupendwa na kupewa mahitaji ya msingi. | | |
| (v) | Kufanya kazi za shule. | | |

Swali lilitoka katika umahiri mkuu *Kuwa Mwadilifu* kwenye umahiri mahususi *Kusimamia Haki.* Swali hili liligawanyika katika vipengele vinne ambavyo vilimtaka mwanafunzi kubainisha matendo yanayoonesha haki au wajibu. Kila kipengele cha swali hili kilikuwa na alama 2. Kwa ujumla kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa wastani ambapo asilimia 66. 2 ya wanafunzi 1,301,560 walikuwa na kiwango cha wastani hadi kizuri sana cha kufaulu, kati yao asilimia

30.4 walikuwa na kiwango cha wastani cha alama 4, asilimia 21.6 kufaulu kuzuri sana kwa alama 8, na asilimia 14.1 kufaulu kuzuri kwa alama 6. Aidha, asilimia 33.9 ya wanafunzi walipata kiwango hafifu cha alama 0 au 2. **Chati Na. 4** inaonesha takwimu za kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 4***: inaonesha ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 66.2 ya wanafunzi walipata alama 4 hadi 8.*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa sababu mbalimbali ziliwafanya wanafunzi kubaini au kushindwa kubaini majibu sahihi kama inavyooneshwa katika uchambuzi ufuatao:

Kipengele (ii) kiliwataka wanafunzi kubaini endapo kitendo cha *kucheza michezo mbalimbali* kinaonesha *Haki* au *Wajibu*. Wanafunzi walioweza kuonesha jibu sahihi *Haki* waliweza kubaini tofauti zilizopo kati ya matendo ya *haki* na *wajibu*. Wanafunzi hao waliweza kutambua kuwa haki ni kitu muhimu sana ambacho mtu au kikundi cha watu wanapaswa kupewa kama vile kuishi, kupata elimu na malezi bora; na

kwa hiyo kucheza michezo mbalimbali ni haki ya kila mtoto. Baadhi ya wanafunzi walioweka alama ya vema kwenye kipotoshi *Wajibu* hawakujua kwamba kucheza michezo mbalimbali siyo wajibu bali ni haki ya mtoto. Wajibu ni majukumu ambayo mtu anapaswa kuyatimiza kama vile kuwatii na kuwaheshimu wengine. Vilevile wapo wanafunzi wengine ambao hawakuelewa matakwa ya swali, kwani waliweka alama ya vema kwenye maeneo yote ya haki na wajibu na wengine kuacha nafasi wazi.

Kipengele (iii) kiliwataka wanafunzi kubaini endapo kitendo cha *Kuwasaidia wakubwa na wadogo zao* kinaonesha *Haki a*u *Wajibu*. Wanafunzi walioweza kuonesha jibu sahihi *Wajibu* waliweza kutambua kuwa mtoto katika jamii ana wajibu wa kuwasaidia watu wengine iwe wakubwa au wadogo katika shughuli mbalimbali za nyumbani au za kijamii kama vile kuosha vyombo na kushiriki katika usafi wa mtaa. Wanafunzi walioweka alama ya vema kwenye kipotoshi *Haki* hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kutofautisha vitendo vya Haki na Wajibu, na kwamba *kuwasaidia wakubwa na wadogo* si kitendo cha haki mtu kufanyiwa bali anapaswa kuwafanyia wengine.

Kipengele (iv) kiliwataka wanafunzi kubaini endapo kitendo cha *Kupendwa na kupewa na mahitaji ya msingi* kinaonesha *Haki* au *Wajibu*. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi *Haki* walikuwa na uelewa kuhusu matendo ya haki za watoto. Wanafunzi hao waliweza kufahamu kuwa watoto wanahitaji kupendwa na kupewa mahitaji muhimu kutoka kwa wazazi, walezi, walimu na wanajamii wote kwa ujumla. Aidha, baadhi ya wanafunzi walioweka alama ya vema kwenye kipotoshi *Wajibu* hawakuelewa kuwa wajibu ni kitu ambacho mtu anatakiwa kukifanya na siyo kupewa. Wengine hawakuwa na uelewa wa stadi muhimu za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na hivyo

kuandika maneno yasiyoeleweka katika vyumba vyote vya Haki na Wajibu.

Kipengele (v) kiliwataka wanafunzi kubaini endapo kitendo cha *Kufanya kazi za shule* kinaonesha *Haki* au *Wajibu.* Wanafunzi walioweza kuweka vema katika upande sahihi wa *Wajibu* waliyafahamu majukumu sahihi ya wanafunzi shuleni kama kusoma kwa bidii, kutunza vifaa vya shule, kuhudhuria shuleni kila siku, kuwaheshimu walimu na wazazi na kufanya kazi za shule. Kwa upande mwingine, wanafunzi walioweka alama ya vema kwenye kipotoshi *Haki* walikosa maarifa juu ya majukumu ya wanafunzi shuleni na hivyo kuchanganya na vitendo vya haki.

**Swali la 5:** Swali hili liliwataka wanafunzi kuchunguza picha na kisha kujibu maswali yanayofuata.



**Maswali**

(i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?

________________________________________

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?

________________________________________


(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kama inavyoonekana katika picha kinaonyesha nini?

________________________________________

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?

________________________________________

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kudumisha Amani* kwenye umahiri mahususi *Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti*. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kuchunguza vitendo vya kuheshimu tofauti za kiutamaduni na kujenga urafiki unaofaa. Kwa ujumla kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani ambapo asilimia 40.9 ya wanafunzi wote 1,301,619 waliofanya swali hili walipata alama 4, asilimia 19.2 walipata alama 6; na asilimia 6.0 walipata alama zote 8; wakati asilimia 33.9 walipata kiwango hafifu cha alama kati ya 0 au 2 kama inavyoonekana katika **Chati Na. 5**.




**Chati Na. 5:** *inaonesha ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwa kuwa asilimia 66.1 ya wanafunzi walipata kati ya kiwango cha wastani hadi kizuri sana cha kufaulu.*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa sababu mbalimbali ziliwafanya wanafunzi waweze kubaini/kushindwa kubaini majibu sahihi kama inavyooneshwa katika uchambuzi ufuatao:

(i) Watu wanaonekana katika picha wanafanya tendo gani?

………………………………………………………………

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuainisha vitendo mbalimbali vya asili na tamaduni ikiwa ni pamoja na kucheza ngoma za asili. Wanafunzi wengi waliweza kubaini na kuandika jibu sahihi *wanacheza ngoma ya asili* au *wanacheza ngoma*. Hii ni kwa sababu ya kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu asili na tamaduni mbalimbali na hivyo kutafsiri picha iliyotolewa kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache walioshindwa swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vitendo vya asili na tamaduni na hivyo kushindwa kubaini kitendo kinachoonekana katika picha. Wanafunzi wengine hawakuwa na stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) hivyo kuandika maneno yasiyoeleweka na baadhi yao kutojaza jibu lolote.

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?

……………………………………………………………..

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini vifaa mbalimbali vya asili vinavyotumika katika ngoma mbalimbali. Wanafunzi wengi waliweza kuchunguza picha na kubaini jibu sahihi ambalo ni *ngoma*. Wanafunzi hao waliashiria kuwa na uelewa wa kutosha juu ya ala mbalimbali za muziki asilia kama ngoma, manyanga na filimbi. Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa swali hili baadhi yao walionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ngoma za asili jambo lililopelekea kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika “umuhimu wa kujifunza vitendo” na wengine waliacha nafasi wazi.


(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kama inavyoonekana katika picha kinaonyesha nini?

…………………………………………………………………….

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini vitendo vinavyopelekea kudumisha amani katika jamii ikiwa ni pamoja na kushirikiana na watu wenye asili tofauti katika mambo mbalimbali kama kusafiri, kusoma, kucheza na kusherekea pamoja. Wanafunzi walioweza kuandika jibu sahihi *uhusiano mwema au uhusiano mzuri* walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayopatikana katika hali ya usalama na utulivu kama vile uhusiano mzuri kati ya watu wenye asili tofauti kama wazungu, wahindi na waarabu.

Hata hivyo, wanafunzi walioshindwa swali hili baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo yanayopelekea hali ya usalama na utulivu na hivyo kuandika majibu ambayo hayakuwa na uhusiano na swali kama "kama ni video kwa nini wanaangalia" na "ngoma na watu". Aidha wanafunzi wengine hawakuwa na stadi za KKK na hivyo kuandika maneno yasiyoeleweka kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5.1**.

**Kielelezo Na. 5.1**


**Maswali**

(i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?

(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kama inavyoonekana katika picha kinaonyesha nini?

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa kuandika maneno yasiyoeleweka.

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?

……………………………………………………………

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi katika kutambua faida za kuishi vizuri na watu wenye asili tofauti. Wanafunzi wengi walioshindwa swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuwa na mahusiano mazuri na watu wenye asili tofauti kama wazungu na wahindi na hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi kama "Kua ni kujisomea vitabu", "Kiti" na "kuwa na afya bora". Aidha wanafunzi wengine walioshindwa swali hili hawakuwa na stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka na wengine kuacha nafasi wazi.

Kwa upande mwingine wanafunzi walioweza kuandika jibu sahihi *kulinda, kuendeleza/kufundisha utamaduni wetu* walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kuwa na mahusiano mazuri na watu

wenye asili tofauti ikiwa ni pamoja na kusoma, kusafiri, kucheza na kusherehekea pamoja. **Kielelezo Na. 5.2** ni sampuli ya mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo Na. 5.2**

**Maswali**

(i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?

wanacheza Ngoma za asili

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?

Ngoma

(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kama inavyoonekana katika picha kinaonyesha nini?

Ushirikiano Kati ya Kabila mbalimbali

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?

ili Kudumisha mila na destuli na Kabila mbalimbali

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuchunguza picha na kuandika majibu sahihi kwa vipengele vyote vinne.

Kwa upande mwengine, wapo wanafunzi walioshindwa kuchunguza picha na kisha kuandika majibu ambayo si sahihi kama ilivyochambuliwa katika kipengele (i) – (iv). **Kielelezo Na. 5.3** kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo Na. 5.3**

**Maswali**

(i) Watu wanaoonekana katika picha wanafanya tendo gani?

Wachezaji

(ii) Ni kifaa gani cha muziki kinachoonekana kwenye picha?

video

(iii) Kitendo cha Wazungu kushirikiana na Waafrika kama inavyoonekana katika picha kinaonyesha nini?

kama ni video kwanini wanaangalia

(iv) Nini umuhimu wa kujifunza kitendo kinachoonekana kwenye picha?

kua ni kujisomea kitaba


**Kielelezo Na. 5.3:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika majibu ambayo hayana uhusiano na maswali aliyoulizwa.

**Swali la 6**: Swali hili liliwataka wanafunzi kusoma kwa makini kifungu cha habari kisha kujibu maswali.

Kifungu cha habari kilikuwa kama ifuatavyo:

*Amina ni mwanafunzi wa Darasa la Nne katika shule ya msingi Kibo. Amina anaishi na shangazi yake ambaye ni tajiri sana. Siku zote Amina huenda shuleni bila kula chochote asubuhi wala kupewa kitu cha kula wakati wa mapumziko kwa sababu ya uchoyo wa shangazi yake. Siku moja rafiki yake aitwaye Joani alimshawishi ili amwibie fedha shangazi yake. Amina alikataa na kumwambia rafiki yake kuwa kuiba sio njia ya kutatua matatizo yake. Amina aliendelea kusema, "Naamini iko siku moja nitafanikiwa kwa kufanya bidii katika masomo yangu na shughuli nyingine, halafu nitajitegemea na kuwasaidia wengine".*

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kuwa Mstahimilivu* na kwenye umahiri mahususi *kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya*. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini tabia zinazobainisha hisia na mtazamo chanya na tabia ya kujifunza katika vikundi. Kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kulikuwa ni kwa wastani ambapo asilimia 11.5 ya wanafunzi 1,301, 559 waliofanya swali hili, walikuwa na alama 8 kati ya 8, asilimia 22.2 walikuwa na alama 6; na asilimia 26.1 walikuwa na alama 4; wakati asilimia 40.2 walikuwa na alama 0 au 2 kama inavyoonekana katika **Chati Na. 6**.




**Chati Na. 6:** *inaonesha ufaulu katika swali la 6 ulikuwa ni wa wastani kwa kuwa asilimia 59.8 ya wanafunzi walipata kati ya alama 4 hadi 8.*

Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kubaini au kushindwa kubaini jibu sahihi kulisababishwa na sababu mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye uchambuzi ufuatao:

(i) Shangazi yake Amina ana tabia gani?

……………………………………………………………..

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kubaini tabia ya shangazi yake Amina. Wanafunzi walioweza kuandika jibu sahihi *uchoyo* au *ubinafs*i walikuwa na maarifa juu ya tabia zisizofaa katika jamii ambazo ni uchoyo, wizi, uvivu, uongo na tamaa. Wanafunzi hao waliweza kutambua kuwa tabia ya shangazi yake Amina ya kutompa Amina kitu chochote anapokwenda shuleni asubuhi ni tabia ya uchoyo. Kwa upande mwingine wanafunzi walioshindwa, baadhi yao waliandika maelezo yasiyohusiana na swali kama “Anacheza Ngoma", "ni tajiri sana", "alikataa" na "anaishi na shangazi yake”. Wakati wengine walionesha kutozimudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) hali iliyopelekea kushindwa kusoma kifungu cha habari na hivyo kuandika mambo yasiyoeleweka kama “kakwi na ynkiwa” na wengine waliacha nafasi wazi.

(ii) Kwa nini Joani hakuwa rafiki mzuri?

…………………………………………………….

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kubaini sababu zinazomfanya Joani asiwe rafiki mzuri. Wanafunzi walioweza kubaini na kuandika jibu sahihi *Kwa sababu alimshawishi Amina amwibie Shangazi yake* walisoma na kukielewa kifungu cha habari na ilikuwa rahisi kwao kutambua jibu sahihi. Wanafunzi hao pia walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya sifa za rafiki mzuri na mbaya. Aidha wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi walikosa maarifa katika kusoma kifungu cha habari walichokuwa wamepewa na hivyo kuandika

majibu yasiyohusiana na swali kama “Tabia Nzuri", "Anacheza ngoma kwa nini", "matatizo", na "fetha Shangazi’.

(iii) Nani alikuwa na mtazamo chanya kati ya Amina na Joani?

…………………………………………………………………

Swali hili lilipima maarifa aliyoyapata mwanafunzi kwenye kifungu cha habari kuhusu mtu mwenye mtazamo chanya kati ya Joani na Amina. Wanafunzi walioweza kubaini na kuandika jibu sahihi *Amina* walisoma kwa makini kifungu cha habari na kukielewa. Wanafunzi hao walionesha uelewa wa kutosha kuhusu hatua alizozichukua Amina kutatua matatizo aliyokuwanayo kama vile kuwaelewa watu wenye tabia tofauti kama Joani. Vilevile walitambua kwamba Amina alikuwa na matarajio ya kufikia malengo yake kwa kujituma. Aidha, wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi walikosa stadi muhimu za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) hivyo ilikuwa vigumu kwao kuelewa maarifa lengwa ndani ya kifungu cha habari na hatimaye kuandika majibu yasiyo na uhusiano na swali na yasiyoeleweka.

(iv) Nani mwenye tabia inayofaa kuigwa kati ya shangazi, Amina na Joani? Toa sababu moja

………………………………………………………………

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kutambua tabia zinazofaa na zisizofaa ambazo zimeainishwa katika kifungu cha habari. Wanafunzi walioweza kusoma kwa umakini kifungu cha habari na kuandika jibu sahihi *Amina* walionesha ufahamu wa kutosha wa kutofautisha matendo yanayofaa na yasiyofaa katika jamii. Wanafunzi hao walitoa sababu mbalimbali zikiwemo “Amina alikataa kuiba fedha toka kwa

shangazi yake", "alikuwa na mtazamo chanya" na "alifanya bidii kwenye masomo".

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi hawakuwa makini wakati wa kusoma kifungu cha habari na hivyo kushindwa kuelewa mahitaji ya swali ambapo baadhi yao waliandika majibu ambayo hayakukamilika kama vile "pamoja na kujisomea" na "Joani ana tabia".

**Kielelezo Na. 6.1** ni sampuli ya majibu mazuri ya mwanafunzi katika Swali la 6.

**Kielelezo Na. 6.1**

**Maswali**

(i) Shangazi yake Amina ana tabia gani?

ya uchoyo

(ii) Kwa nini Joani hakuwa rafiki mzuri?

Kwa sababu alimshawishi Amina amwibie shangazi yake.

(iii) Nani alikuwa na mtazamo chanya kati ya Amina na Joani?

Ni Amina

(iv) Nani mwenye tabia inayofaa kuigwa kati ya Shangazi, Amina na Joani?

Toa sababu moja.

Amina ni mwenye tabia inayofaa kuigwa; kwa sababu yeye ni mtoto mwenye tabia nzuri au ajema na mtiifu Joani alimshawishi amwibie shangazi yake lakini Amina alikataa na akasema kuiba si kufata maelekezo yake

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeelewa matakwa ya kila swali na hivyo kutoa majibu sahihi kwa vipengele vyote vinne.

Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kusoma kifungu cha habari kwa makini na hivyo kuandika majibu ambayo si sahihi kama

ilivyochambuliwa katika kipengele (i) – (iv). **Kielelezo Na. 6.2** kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo Na. 6.2**

**Maswali**

(i) **Shangazi yake Amina ana tabia gani?**

anaishi na shangazi

(ii) **Kwa nini Joani hakuwa rafiki mzuri?**

fetha shangazi

(iii) **Nani alikuwa na mtazamo chanya kati ya Amina na Joani?**

kujisomea shuleni

(iv) **Nani mwenye tabia inayofaa kuigwa kati ya Shangazi, Amina na Joani?**

**Toa sababu moja.**

kuandika na kujisomea shuleni

kulima

Pamoja na kujisomea

Shuleni na kujisomea

**Kielelezo Na. 6.2:** Kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambayo hayana uhusiano na maswali aliyoulizwa mfano; fetha shangazi, kulima n.k.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la 06 Uraia na Maadili unaonesha kuwa baadhi ya umahiri ulikuwa na ufaulu mzuri na baadhi ulikuwa na ufaulu wa wastani. Kwa ujumla, ufaulu kwa wanafunzi katika umahiri wote ulikuwa mzuri. Aidha, umahiri wa *Kuthamini Jamii* kwa Swali la 1 ulikuwa na kufaulu kwa asilimia 93.2, umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* kwa Swali la 3 ulikuwa na kufaulu kwa asilimia 79.1. Vile vile, umahiri wa

*Kuwa Mwadilifu* kwa Swali la 4 ulikuwa na kufaulu kwa asilimia 66.1, *Kudumisha Amani* kwa Swali la 5 ulikuwa na kufaulu kwa asilimia 66.1, *Kuwa Mstahimilivu* kwa Swali la 6 kulikuwa na kufaulu kwa asilimia 59.8 na *Kuheshimu Jamii* kwa Swali la 2 ulikuwa na kufaulu kwa asilimia 45.1. Taarifa zaidi za kufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri zimeoneshwa katika kiambatisho A na B.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulionesha kuwa, kwa ujumla wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri ambapo asilimia 92.80 ya wanafunzi walipata kiwango cha wastani hadi kizuri sana cha daraja A hadi daraja D na wanafunzi wachache (7.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata daraja E. Umahiri wote ulipimwa ambao ni *Kuthamini Jamii*, *Kuheshimu Jamii*, *Kuwa Mwajibikaji*, *Kuwa Mwadilifu*, *Kuwa Mstahimilivu* na *Kudumisha Amani*. Umahiri wa Kuthamini Jamii na Kuwa Mwajibikaji ulikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Umahiri uliobaki ulikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu.

Uchambuzi ulionesha kuwa kufanikiwa katika upimaji kumechangiwa na uwezo mzuri wa wanafunzi kujua mahitaji ya swali, maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa na kuwa na stadi za ufahamu. Pia walimudu vyema stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Pamoja na mafanikio hayo, wanafunzi wachache walipata alama za chini kwa sababu ya kutokuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa, kukosa stadi za KKK na hivyo kushindwa kujua mahitaji ya swali na kuandika sentensi zisizoeleweka. Pia walionesha kukosa stadi za ufahamu na hivyo kushindwa kujibu swali la ufahamu kwa usahihi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu waongeze juhudi katika kufundisha umahiri wote ulioainishwa katika muhtasari na hasa ule wenye viwango vya wastani vya kufaulu.

(b) Walimu wawafundishe wanafunzi kusoma vizuri mahitaji ya swali kabla ya kujibu.

(c) Wanafunzi wanatakiwa kuhamasishwa kusoma vitabu vya kiada na rejea ili kuongeza uelewa wao katika umahiri mbalimbali wa somo hili.

(d) Walimu waandae majaribio na mitihani inayokuza uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayopima stadi mbalimbali.

(e) Walimu wa somo la Uraia na Maadili wapewe mafunzo maalumu ili kuwaboreshea uwezo wa kulifundisha somo hili utakaowasaidia kupima kwa usahihi viwango vya utendaji vya wanafunzi shuleni.

(f) Walimu wafanye jitihada ili kuwasaidia wanafunzi kuboresha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) pamoja na zile za ufahamu.

**Kiambatisho A**

## UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

| Na | Umahiri | UPIMAJI WA 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila swali | | Wastani wa kufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % za kufaulu | | |
| 1 | Kuthamini Jamii | 1 | 93.2 | 93.2 | Nzuri |
| 2 | Kuwa Mwajibikaji | 3 | 79.1 | 79.1 | Nzuri |
| 3 | Kuwa Mwadilifu | 4 | 66.2 | 66.2 | Wastani |
| 4 | Kudumisha Amani | 5 | 66.1 | 66.1 | Wastani |
| 5 | Kuwa Mstahimilivu | 6 | 59.8 | 59.8 | Wastani |
| 6 | Kuheshimu Jamii | 2 | 45.1 | 45.1 | Wastani |

**Kiambatisho B**

# MUHTASARI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI

